Missouri Inahesabiwa:

Mwongozo wa Ujumbe wa Sensa ya 2020

Imetayarishwa na Missouri Foundation for Health

Machi 2020 | Kiswahili

Ujumbe Muhimu

Sensa ya 2020 ni nafasi yetu ya kuhakikisha kuwa dola za ushuru zilizopatikana kwa jasho ambazo tunatuma Washington, D.C. zinarudi Missouri. Kwa kila mtu mzima na kila mtoto ambaye hahesabiwi katika sensa, jimbo letu litapoteza dola za serikali kuu $1,300 kila mwaka. Wakati kila mkazi wa Missouri anahesabiwa, tunapata pesa zaidi kwa ajili ya kutengeneza barabara na madaraja, hospitali na shule. Hesabiwa kwenye Sensa ya 2020 leo kwenye my2020census.gov. Kwa sababu Missouri Inahesabiwa!

Hatari Iliyopo

- Sensa hufanyika kila baada ya miaka 10. Endapo sote hatutahesabiwa 2020, Missouri itatamaushwa kwa mwongo ujao.
- Kwa kila mtu mzima na kila mtoto ambaye hahesabiwi katika sensa, jimbo letu litapoteza dola za serikali kuu $1,300 kila mwaka kwa kila mtu kwa zaidi ya miaka 10 ijayo. Hizo ni fedha ambazo hatutapata kwa ajili ya kutengeneza barabara na madaraja, hospitali na shule zetu.
- Mwaka wa 2010, Missouri ilipoteza kiti katika Bunge la Marekani kwa sababu si kila mtu alihesabiwa. Hatuwezi kuhatarisha kupoteza sauti nyingine ya Missouri huko Washington, D.C.

Umuhimu Wake

- Sote tukihesabiwa, Missouri inapata pesa zaidi za kuboresha barabara na kujenga upya madaraja yetu.
- Sote tunapohesabiwa, mipango yetu ya huduma ya afya na vituo vya afya vya jamii vinapata fedha zaidi za kushughulikia familia, marafiki na majirani wetu. Tunapokosa kuhesabiwa sote, hospitali zinaweza kupoteza hela na hivyo kulazimisha watu kusafiri kwa muda mrefu kupata huduma.
- Sote tunapohesabiwa, shule zetu hupata fedha muhimu za kushughulikia watoto wetu. Hii inajumuisha mipango ya baada ya kutoka shuleni na vyakula vya mchana vya watoto.

Hoja Muhimu kwa Wahamiaji

- Kuhesabiwa katika sensa ni sehemu ya wajibu wetu wa raia.
- Sensa haitakuuliza ikiwa wewe ni raia wa Marekani. Kila mtu anayeishi Marekani, bila kujali hali ya uraia au uhamiaji, anapaswa kuhesabiwa katika sensa.
- Sensa itapatikana kwa lugha nyingi. Sensa itapatikana mtandaoni na simu katika lugha 13, ikiwemo Kiswahili. Toleo la karatasi la kutuma barua litapatikana kwa Kiingereza na Kihispania.
- U.S. Census Bureau itahifadhi taarifa zako kwa faragha. Hawaruhusiwi kushiriki taarifa zako na yeyote, ikiwemo mashirika mengine ya serikali.
- Ukijibu sensa wakati unaofaa, huenda mfanyakazi wa sensa asije nyumbani kwako. Njia rahisi ya kujibu ni mtandaoni kwenye my2020census.gov au kwa simu. Hata unaweza kutumia simu ya kisasa.
- Hakikisha kuwa umemhesabu kila mtu anayeishi kwenye nyumba au chumba chako. Haijalishi ikiwa hajaorodheshwa kwenye makubaliano ya kupangisha. U.S. Census Bureau haiwezi kushiriki taarifa zako na mwenye nyumba wako.

Wazazi na Walezi wa Watoto Wachanga

- Amini usiamini, watu wengi husahau kuhesabu watoto walio nyumbani mwao. Kila mtu anahesabiwa na ni muhimu kuwahesabu watoto wa umri wote, ikiwemo wapwa, binamu na wajukuu. Usisahau kuhesabu wadogo wako zaidi. Hawa ni pamoja na watoto waliozaliwa, hata ikiwa bado wako hospitalini.

Maswali Yanayoulizwa Sana

Sensa ni nini?

- Sensa ni hojaji — chukulia tu kama utafiti. Inauliza maswali tisa pekee. Huhesabu kila mtu mzima na mtoto wanaoishi Marekani. Hufanyika kila baada ya miaka 10. Sensa ijayo itafanyika 2020.
- Sensa husaidia serikali kutambua kiasi cha pesa ambacho kila jimbo linapata kwa mipango muhimu. Sensa pia huamua uwakilishaji wa kila jimbo katika Bunge la Marekani.
- Sensa ni sehemu ya Katiba ya Marekani. Ni wajibu wa raia wa kila mtu kujibu.

Sensa huuliza nini?

- Sensa huuliza maswali tisa rahisi kuhusu watu wanaoishi katika nyumba yako. Hii ni pamoja na majina, umri, mbari, jinsia na ikiwa unamiliki au kupangisha nyumba yako.
- Sensa haitauliza mapato yako wala chama cha siasa.
- Sensa haitauliza ikiwa wewe ni raia. Huenda ulisikia kuhusu hili kwenye habari. Mwishoni, swali hili halikuongezwa.

Itafanyika lini?

- Sasa hivi! Unaweza kutarajia kupata maagizo kutoka U.S. Census Bureau katika barua au katika baadhi ya jamii za vijijini, kuwasilishwa nyumbani kwako kwa mkono mapema Machi 2020. Unaweza kujibu mtandaoni kwenye my2020census.gov au kwa simu.
- Ukijibu sensa wakati unaofaa, huenda mfanyakazi wa sensa asije nyumbani kwako.

Ni nani anayehitaji kujibu?

- Ni muhimu kwa kila mtu mzima na kila mtoto aliye Missouri kuhesabiwa. Hawa ni pamoja na watoto, bibi/babu au wanafamilia wengine na watumiaji wa chumba kimoja wanaoishi nyumbani kwako.
- Unapaswa kujibu bila kujali hali yako ya uraia au uhamiajio.

Ninaweza kujibu vipi?

- Unaweza kujibu leo kwenye my2020census.gov. Unaweza kufanya hivyo kupitia kompyuta au kwenye simu yako ya mkononi.
- Pia unaweza kuwasiliana na U.S. Census Bureau ili kujibu maswali ya sensa.
- Familia nyingine zitapata maswali ya sensa kupitia barua au kuwasilishwa nyumbani kwao kwa mkono. Hii ni kwa sababu huenda wasiwe na intaneti ya kutosha au ni wazee wanaoishi nyumbani.
- Sensa inapatikana kwa lugha nyingi. Sensa inapatikana mtandaoni na simu katika lugha 13, ikiwemo Kiswahili. Toleo la karatasi la kutuma barua linapatikana kwa Kiingereza na Kihispania.

Je, taarifa yangu iko salama?

- Ndiyo, taarifa yako ni salama. U.S. Census Bureau itahifadhi taarifa yako kwa faragha.
- Ni haramu kwa U.S. Census Bureau kushiriki taarifa yako na mashirika mengine ya serikali, mahakama au kampuni za binafsi.
- Mfanyakazi wa sensa hatawahi kukuomba nambari yako ya Usalama wa Jamii wala taarifa kuhusu akaunti za benki wala kadi zako za mikopo. U.S. Census Bureau haitakutumia barua pepe kuhusu Sensa ya 2020.
- Ikiwa unataka kuhakikisha kuwa mtu aliye mlangoni pako ni mfanyakazi wa sensa, angalia beji yake. Wafanyakazi wote wa sensa wana beji rasmi ya kitambulisho cha U.S. Census Bureau. Beji inapaswa kujumuisha jina, picha, alama ya mwanga ya Idara ya Biashara na tarehe ya mwisho. Pia atakuwa amebeba mkoba rasmi wenye nembo ya Census Bureau na barua rasmi inayoelezea sababu ya kuja nyumbani kwako.

Je, sensa inauliza kuhusu uraia?

- La, sensa haitauliza ikiwa wewe ni raia wa Marekani. Huenda ulisikia kuhusu hili kwenye habari. Mwishoni, swali hili halikuongezwa.